Kuwalipa walimu bahshishi kwa matokeo ya kujifunza:

Kuwahamasisha walimu kuboresha kujifunza katika madarasa ya I, II na III

1. Utangulizi

Watoto wote wanapaswa kujifunza kusoma na kufanya hesabu vizuri katika miaka yao ya mwanzo ya shule ya msingi, na ni walimu wenye jukumu la kuhakikisha jambo hili linafanikiwa. Kuonesha kwamba kujifunza ni muhimu na kuwatia moyo walimu kuwasaidia watoto kujifunza, Twaweza ilianzisha “Malipo Kwa Walimu baada ya Matokeo”, mfumo mpya wa kuwahamasisha walimu. Katika mfumo huu, Twaweza iliahidi kuwalipa walimu wa darasa la I, II na III kutegemeana na stadi ambazo wanafunzi wao wamejifunza. Malipo haya ni nyongeza kwenye mshahara wa kawaida wa mwalimu, na hakuna adhabu pale ambapo mwalimu hatapata matokeo mazuri. Mfumo huu wa Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo, unatoa fursa kwa walimu kupata kipato zaidi pale wanafunzi wao wanapofanya vizuri.

KiuFunza ni utafiti wa majaribio unaopima matokeo kwa kutoa huduma kwa kundi moja na kulinganisha na kundi lilingine lisilopewa huduma: Hii ina maana kwamba bahshishi hutolewa kwenye kundi moja la shule huku

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
s: +255 22 266 4301, | bp: info@twaweza.org |
www.twaweza.org/kiufunza

KiuFunza

Twaweza ni sisi

kundi lingine likiachwa kwa makusudi bila kupewa bahshishi – kundi la kuthibitisha. Kipengele muhimu ni kwamba shule zilizopo kwenye mpango huu zilichaguliwa kinasibu. Hii ina maana kuwa kwa wastani shule zilizochaguliwa kwenye mpango huu na shule za kuthibitisha zote zilikuwa katika nafasi "sawa" kabla ya kuanza. Hivyo kuna uwiano sawa kati ya shule zinazopata bahshishi na zisizopata.

2. Maswali kumi ya msingi kuhusu Malipo Kwa Walimu baada ya Matokeo

Swali la 1: Je, kwa nini ni muhimu kuboresha kujifunza katika shule za msingi?

Elimu bora ndio njia ya kuleta mafanikio ya kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja, na kwa Tanzania kwa ujumla. Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi kufikia karibu wanafunzi milioni 4, yaani kutoka wanafunzi milioni 4.4 mwaka 2000 na kufikia wanafunzi milioni 8.3 mwaka 2012. Rasilimali nyingi za kibajeti zinahitajika kukidhi mahitaji ya ongezeko hili. Inatarajiwa kuwa kutakuwa na ongezeko la ziada la wanafunzi kutokana na kukua kwa idadi ya watu nchini: walimu wenye umahiri wa kufundisha wanapaswa kuajiriwa na kupewa mafunzo ili kuhakikisha kuwa watoto wetu wanajifunza stadi za msingi za kusoma na kuhesabu. Bila stadi hizi, mtoto hataweza kufikia elimu ya sekondari na chuo kikuu.

Leo hii, watoto wengi wanapata shida kujifunza stadi hizi za msingi. Takwimu za tathmini ya Uwezo zinaonesha kuwa viwango vya ufaulu kwa kutumia majaribio ya darasa la II miongoni mwa watoto wenye miaka 10-16 ni asilimia 56 katika kusoma hadithi ya Kiswahili, asilimia 35 katika kufanya hesabu za kuzidisha na asimila 13 tu katika kusoma hadithi ya Kingereza (Uwezo ni tathmini kubwa ya kupima watoto kujifunza; haya ni matokeo ya 2015). Kwa kuwa watoto hawa wameshavuka darasa la 2, takwimu za Uwezo zinaonyesha kuwa watoto hawajifunzi ipasavyo katika madarasa ya awali. Hali hii inahatarisha hali kujifunza maishani na huwakosesha Watanzania fursa za ajira katika soko huru la ajira.

Swali la 2: Je, motisha kwa mwalimu ina umuhimu gani?

Watafiti na wataalamu wa elimu wanakubaliana kuwa walimu ndio nguzo muhimu katika mchakato mzima wa kujifunza. Hata hivyo, tatizo kubwa lililopo ni kwamba walimu hawahudhurii madarasani ipasavyo. Hapa Tanzania, idadi kubwa ya walimu hawaingii madarasani kufundisha.

Tumeyajuaje haya? Taarifa za walimu kutokuhudhuria madarasani zimepatikana kutokana na ziara za kushitukiza mashuleni. Watafiti wa KiuFunza walitembelea shule wakiwa na orodha ya majina ya walimu na masomo wanayofundisha kwa madarasa ya I, II na III. Watafiti walithibitisha kama je, mwalimu alipokuwapo shuleni? Na pia je, alikuwa anafanya nini?

Kielelezo cha 3 kinaonesha matokeo ya "mwalimu wangu yupo wapi?" kutokana na ziara hizo za kushitukiza kwa mwaka 2015 na 2016. Kielelezo hiki kinaonesha kuwa mwaka 2016 mahudhurio ya mwalimu madarasani yalikuwa mazuri kuliko mwaka 2015, lakini bado ni asilimia 54 tu ya walimu waliokuwa kazini. Kwa sababu utafiti huu una uwakilishi wa kitaifa, maana yake ni kwamba katika shule zote za umma katika madarasa ya I, II na III, asilimia 46 ya walimu hawakuwepo madarasani mwezi Julai/Agosti 2016. Matokeo haya yanathibitishwa na

tafiti nyingine za kitaifa, kwa mfano utafiti wa Viashiria vya Utoaji Huduma (Service Delivery Indicators), wa mwaka 2014 unaonesha kuwa asilimia 47 ya walimu hawakuwa madarasani.

Kielelezo cha 1: Mwalimu wangu yupo wapi?



Takwimu zinatoka shule za msingi za umma, darasa la 1-3 (2015-16)
Chanzo: *Twaweza KiuFunza* 2015 na 2016 utafiti wa kati wa mahudhurio ya walimu.

Hali hii ya mahudhurio hafifu ya walimu kazini inasababisha hasara kubwa mbili. Kwanza, watoto wengi hutumia muda wao darasani bila kupata mafunzo wanayostahili ya stadi za msingi. Pili, serikali ya Tanzania pamoja na walipa kodi wanawalipa walimu mishahara kamili kila mwezi kwa huduma ambayo haikutolewa kikamilifu na walimu.

Tuichambue hasara ya pili iliyotajwa hapo juu. Zingatia kwamba walimu wa madarasa ya I, II na III kwa wastani hulipwa shilingi milioni 9 kwa mwaka (kutokana na fidia kabla ya makato ya kodi, kama walivyosema walimu). Kwa kutumia kigezo kuwa asilimia 46 hawakuwepo madarasani, walipa kodi wamepoteza shilingi milioni 4.1 kwa mwaka kwa kila mwalimu ambaye alipaswa kuwa akifundisha lakini hakuwepo darasani. Haya ni makadirio ya chini kabisa kwani gharama iliyoanishwa ni kwa walimu wa madarasa ya I, II na III, lakini ukweli ni kwamba madarasa haya na madarasa ya juu hufundishwa na walimu wakongwe ambao hulipwa mishahara mikubwa zaidi.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia *(Basic Education Statistics – BEST)* za mwaka 2016, Tanzania ilikuwa imeajiri walimu 191,604 katika shule za msingi za umma. Hii ina maana kuwa makisio ya jumla ya hasara kwa mishahara ya walimu ni ***shilingi bilioni 786 kila mwaka***. Ukilinganisha kiasi hiki na shilingi bilioni 306 zilizopotea mwaka 2014 katika kashfa ya IPTL Escrow na kuzua mtafaruku mkubwa nchini, upotevu wa fedha kupitia mishahara ya walimu wa shule za msingi ni mara mbili ya hasara iliyotokana na kashfa hiyo ya Escrow. Na kumbuka kiasi hiki hupotea kila mwaka!

Swali la 3: Je, ni kwa jinsi gani motisha kwa walimu inaweza kuboresha kujifunza?

Katika hili, watunga sera wanakumbana na changamoto kuu mbili: i) kujifunza shuleni kunahitaji maboresho; ii) bajeti ya elimu, hususani mishahara ya walimu, inahitajika kutumika kwa ufanisi zaidi. Nini kifanyike? Twaweza imezifanyia kazi changamoto zote mbili za kujifunza na kuwapa walimu motisha. Tumetumia njia mbalimbali za kuwamotisha walimu kwa kutumia malipo ya fedha baada ya matokeo mazuri ya kujifunza kudhihirika; mfumo ambao unahusisha malipo kwa walimu na stadi ambazo watoto wao wamejifunza.

Lengo la msingi katika elimu ni kuhakikisha *watoto wanajifunza*. Je, kwa nini walimu hawahudhurii madarasani? *Motisha.* Hivyo tulichagua kitu ambacho kihistoria kina uwezo mkubwa wa kumotisha (fedha) na kuihusisha na matokeo ya kujifunza. Haya tumeyaita "**Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo" (*Cash on Delivery* - COD).** Walimu hufundisha na kuzawadiwa **fedha kama bahshishi**.

'Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo' yanawapa walimu ujumbe muhimu kutoka kwa Serikali, (inayowalipa walimu mishahara), kuhusu **umuhimu wa kujifunza**. Vile vile malipo haya yanawatambua walimu wanaofanya jitihada za ziada kuwajali wanafunzi wao. Hivyo **Malipo Kwa Walimu baada ya Matokeo** huonekana wazi na kujenga uwajibikaji wa walimu katika kujifunza kwa wanafunzi wao.

Swali la 4: Je, Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo kumeongeza kiwango cha kujifunza nchini Tanzania?

Ndiyo. Mwaka 2015-16 tumepata matokeo chanya kwenye matokeo ya wanafunzi katika shule ambazo Twaweza ilitoa malipo haya. Hii inamaanisha kuwa tuna uthibitisho kuwa motisha ya fedha inaweza kuwahamasisha walimu kuboresha utendaji wao na kuwasaidia wanafunzi wao kujifunza zaidi.

Katika baadhi ya shule (mwaka 2013-14), Twaweza ilitafiti endapo kuchanganya bahshishi kwa walimu na fedha za ruzuku kwa ajili ya mahitaji ya shule kutaleta matokeo ya kujifunza. Fedha za ruzuku hunufaisha shule nzima, na siyo tu madarasa ya KiuFunza. Pale ambapo bahshishi na ruzuku vilichanganywa, matokeo ya kujifunza katika madarasa ya I, II na III, yalikuwa ni mazuri: tulibaini kuwa viwango vya ufaulu wa Kiswahili na Hesabu viliongezeka kwa asilimia 20 katika kipindi cha mwaka mmoja. Ni tafiti chache sana duniani, zinazopima jitihada kwenye elimu, zilizoonesha matokeo makubwa kama haya.

Utafiti wa KiuFunza unaonesha kuwa utoaji wa fedha za ruzuku bila motisha kwa walimu hauboreshi kujifunza. Lakini fedha za ruzuku zikiambatana na motisha kwa walimu husaidia watoto kujifunza. Matokeo haya ni muhimu kwa sababu bajeti ya elimu ni kubwa na imejikita katika vitendea kazi kama vile mishahara, vitabu, madawati na mahitaji mengine ya shule. Matumizi ya bajeti yanapaswa kufanywa kwa ufanisi kadiri inavyowezekana. KiuFunza inaonesha kuwa motisha inaweza kuboresha thamani ya fedha ya bajeti inayotolewa sasa katika sekta ya elimu.

Zaidi ya hayo, motisha kwa walimu inaweza kuwa na matokeo chanya ya kuwavutia watu wenye vipaji/uwezo kuwa walimu. Vile vile, walimu nchini Tanzania wanakumbana na changamoto za kutokutambuliwa au kukosa fursa, hali inayosababisha watu ambao wangeweza kuwa walimu wazuri kuikimbia taaluma ya ualimu.. **Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo** inaweza kuwavutia watu wenye vipaji kujiunga kwenye sekta hii muhimu.

Swali la 5: Lakini hili ni wazo la "kitaaluma" je, linawezekana kutekelezwa kwa vitendo?

Kimsingi, Tanzania imeshaanza kutekeleza mfumo wa motisha shuleni. Chini ya Matokeo Makubwa Sasa (BRN), mpango huu ulianza kama motisha ya fedha shuleni mwaka 2014. Katika mpango huu, ni shule chache tu zilipata bahshishi, hivyo walimu wengi hawakufikiwa moja kwa moja. Zaidi ya hayo, bahshishi ililipwa kwa shule, na si kwa mwalimu. Hata hivyo, huu ulikuwa mwanzo mzuri kwani inaonesha kuwa utaratibu wa kulipa motisha ni jambo

linalokubaliwa na kwa sasa tayari upo mfumo wa *kupima na kuzawadia matokeo ya kujifunza kwa shule.*

Mfumo wa motisha unaweza ukafananishwa na mfumo wa injini: kwamba mabadiliko ya muundo wake yanaweza kubadili nguvu ya injini. Ni vema tukajaribu miundo mbalimbali kwa sababu inaweza kutupeleka kwenye matokeo tofauti. Maoni yetu ni kuanza kutekeleza malipo ya fedha ya motisha kwa walimu baada ya matokeo, kwa kuanza na sampuli ndogo, na kujifunza kutokana na matokeo tutakayoyapata, ili kuboresha na kujaribu tena, na hatimaye kuchagua muundo wenye tija kubwa kabla ya kuutekeleza kwenye eneo kubwa la nchi.

Utafiti wa Twaweza unaunga mkono muundo ambao:

a. Wanafunzi na walimu wengi zaidi watanufaika;
b. Bahshishi inalipwa moja kwa moja kwa walimu, kama sehemu ya fidia ya huduma yao kwa mwaka.
c. Bahshishi iwe na thamani kwa wastani, na
d. Muundo wa motisha uelezewe kwa ufasaha, kwa walimu na wadau.

Swali la 6: Je, motisha inaweza kutekelezwa katika eneo kubwa, na kwenye maeneo mengine?

Ipo mifano hai ya mifumo ya motisha kwa walimu ambayo hufanya kazi katika eneo kubwa. Mfano mmoja ni nchini Brazili katika jimbo la Pernambuco, ambapo mpango wa motisha uliwafikia walimu 50,000 katika shule 950 na kuleta matokeo ya kujifunza.

Mfano mwingine wa Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo katika ngazi ya kitaifa ni nchini Chile, ambapo shule zote za msingi 6,500 zinazoendeshwa na serikali zilishiriki na matokeo kwenye majaribio ya hisabati na lugha kupatikana.

Tafiti nyingine zilizotekeleza motisha kwa walimu katika kiwango kidogo na kupata matokeo, zimefanyika nchini Kenya, India na Israel. Hitimisho la jumla kwenye tafiti hizi ni kwamba motisha kwa walimu imeboresha kujifunza katika maeneo mbalimbali lakini pia aina ya muundo na taratibu za utekelezaji yana umuhimu mkubwa sana.

Nchini Tanzania, itarajiwe kwamba changamoto nyingi zinaweza kujitokeza katika kutekeleza mfumo wa kuwalipa walimu baada ya matokeo ya kujifunza. Hivyo, ni vizuri kujifunza kwa kutekeleza kwa majaribio kabla ya kutekeleza nchi nzima. Baadhi ya mambo muhimu yanayohitajika kuwepo ni:

- Utayari wa Serikali kupitia Wizara za Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST), Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Fedha na Mipango (FM) kushirikiana na kutenga fedha maalumu kulipia bahshishi hiyo;
- Kuwepo kwa makubaliano kuhusu muundo na utaratibu wa upimaji matokeo ya kujifunza;
- Uongozi wa kusimamia utekelezaji wa utoaji wa motisha;
- Ujumbe rahisi, unaoeleweka na kuaminika na walimu mwanzoni mwa mwaka kuhakikisha kwamba ahadi ya malipo hayo inaeleweka vema; na
- Mawasiliano baada ya malipo kwa ajili ya kupata mrejesho.

Katika kipindi cha nyuma Twaweza ilitekeleza aina mbalimbali za utoaji wa motisha na, kwa msaada wa washirika mbalimbali, **hivyo, ipo tayari kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa mpango wa kuwalipa walimu motisha.**

Swali la 7: Je, ufanywe uamuzi gani kuhusu muundo?

Uamuzi wa Kwanza unahusu swali la **nini:** Je, ni nini hasa kitakachopimwa na kulipiwa? Wachambuzi wengi wa elimu wanakubaliana kuwa kipimo kizuri ni tofauti kati ya kile ambacho mwanafunzi aliweza kufanya kabla, na anachoweza kukifanya baada ya kufundishwa. Hiki ndicho kipimo ambacho mpango wa Utoaji wa Motisha kwa Shule iliyoonesha maendeleo kuliko shule nyingine, (*School Improvemment Grant - SIG*) walitumia ambapo shule hulipwa bahshishi baada ya kupima na kuona kwamba imefanya vizuri zaidi kuliko hapo awali. Faida ya muundo huu ni kwamba hauzipendelei shule ambazo zimekuwa katika nafasi nzuri tangu mwanzo, kwa mfano shule za mijini zenye wanafunzi wenye uwezo mkubwa zaidi.

Uamuzi wa Pili: ni kuhusu mlengwa wa motisha au kujibu swali la **nani**: Je, ni matokeo ya nani yatapimwa? Ya mwalimu mmoja mmoja au makundi ya walimu? Kiutendaji, kutoa motisha kwa kundi na kwa kutumia takwimu za mtihani wa taifa, ni rahisi kutumika na huweza kupunguza gharama.

Uamuzi wa Tatu: ni kuhusu **kiasi** cha bajeti ya motisha. Kiasi cha bajeti kikigawanywa kwa idadi ya watakaonufaika kitatupatia wastani wa malipo ya motisha/ bahshishi. Kiasi cha wastani kikiwa juu, ndivyo matarajio ya matokeo yataongezeka.

Swali la 8: Je, Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo inagharimu kiasi gani?

Ukweli ni kwamba Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo kutaongeza bajeti ya sekta ya elimu, hata hivyo, motisha italipwa endapo tu viwango vya ufaulu vimeongezeka. Hii ina maana kuwa bajeti kwa kila mwanafunzi itaongezeka; kwa kiwango gani, itategemea muundo.

Bahshishi za KiuFunza ambazo zililipwa kwa walimu wa madarasa ya I, II na III pekee, ilikuwa ni karibu asilimia 3 ya bajeti ya sasa kwa kila shule. (Utekelezaji wa Twaweza uliongeza gharama za ziara kwenye shule kwa ajili ya mawasiliano ya awali (karibu asilimia 1) na ziara mwishoni mwa mwaka kuwapima wanafunzi (asilimia 3). Hivyo, kama gharama za upimaji zinaweza kuepukika kwa kutumia takwimu zilizopo za mtihani, gharama ya Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo kwa madarasa ya chini ni karibu asilimia 4 ya bajeti ya sasa.

Lakini tuzingatie kuwa gharama kwa kila mwanafunzi anayefaulu ndilo jambo muhimu la kujali katika mfumo wa elimu: hii ni wastani wa gharama kwa mwanafunzi atakayefanikiwa kufikia malengo ya mtaala, kwa mfano mtihani wa darasa la 4. Gharama kwa kila anayefaulu itashuka endapo jumla ya gharama ya mfumo wa Malipo kwa Walimu bada ya Matokeo kwa kila mwanafunzi wa ziada anayefaulu ni ya chini ya wastani wa gharama ya sasa kwa kila mwanafunzi anayefaulu.

Swali la 9: Vipi kuhusu usawa? Je, serikali itoe malipo tofauti kwa walimu?

Mapendekezo ya Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo sio ya kibaguzi. Kila mwalimu ana haki ya kupata malipo, kutegemena na utendaji wake. Viwango vya malipo ya mshahara

havitaathirika. Kinachoongezeka ni bahshishi kwa utendaji mzuri. Hata hivyo, kwa kuwa lengo ni kuboresha kujifunza katika madarasa ya chini kwa gharama ndogo kadiri iwezekanavyo, kwa KiuFunza bahshishi ilitolewa tu kwa walimu wa madarasa ya I, II na III.

Kama serikali itapenda mfumo huu inaweza kuuanzisha na kujikita kwenye shule za vijijini ambako maisha na mazingira ya kufundishia yana changamoto nyingi na hivyo kutowavutia walimu kwenda kufanya kazi huko. Kwa kuzilenga shule hizi za vijijini, bahshishi inaweza kutumika kuboresha mazingira ya shule hizo ambazo zinahitaji msaada zaidi. Walimu pia watahamasika kwenda kufundisha kwenye shule hizo na kusaidia kuongeza maarifa kwa wanafunzi.

Swali la 10: Je, ni vigumu kutekeleza Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo?

Kuna majukumu matano ya kutekelezwa katika kuendesha mfumo wa Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo. Majukumu hayo yameainishwa kwenye jedwali hapa chini pamoja na mgawanyo wa kazi wakati wa majaribio ya utekelezaji.

Tendo	Nini kinahitajika kifanyike?	Mhusika (anaye pendekezwa)
(1) Mawasiliano	Kuwaeleza walimu kanuni za utoaji bahshishi mwanzoni mwa mwaka, kwa uwazi na ushirikishaji; na kutoa mrejesho kuhusu malipo kwa utendaji mwaka unaofuata na hata kupitia ujumbe mfupi wa simu.	Twaweza
(2) Taarifa za somo la mwalimu na akaunti yake ya benki	Kuandaa orodha ya majina ya walimu wanaoshiriki katika shule kwa madarasa. Taarifa hii iainishe namba ya akaunti ya benki ya kila mwalimu na namba ya simu yaani kuandaa kanzidata ya malipo haya.	TAMISEMI
(3) Takwimu za majaribio ya wanafunzi na ukaguzi	Kuandaa upimaji shuleni na kuweka kumbukumbu ya takwimu za mwanafunzi. *kukagua majaribio kuchunguza matokeo yasiyo ya kawaida	NECTA, TAMISEMI *Twaweza, NECTA
(4) Tengeneza fomu za malipo	Kijumuisha (2) na (3) kutengeneza fomu za kiwango cha bahshisi cha kila mwalimu anayestahili. Fomu hizo ziidhinishwe na Kamati maalumu itakayosimamia Malipo kwa Walimu kwa Matokeo na kupelekwa OR-TAMISEMI. Takwimu zote za shule za viwango vya bahshishi ziwekwe wazi ili walimu waweze kukaguia malipo yao.	Twaweza

(5) kulipa bahshishi	Kutuma malipo. Malipo ya bahshishi yanaweza kulipwa moja kwa moja kwenye akaunti za walimu za mishahara mara baada ya kiwango cha bahshishi kujulikana. *ukaguzi wa sampuli ya malipo kuthibitisha upokeaji	TAMISEMI *Twaweza, TAMISEMI

3. Hitimisho: Je, inawezekana kutekeleza Malipo kwa Walimu baafa ya Matokeo nchini Tanzania?

Elimu ni kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Tano. Hata hivyo, jitihada zilizoanzishwa zinaegemea zaidi katika kuanisha mambo yanayoonekana na yanayohesabika – madawati na maabara n.k. Twaweza inaamini kuwa lazima tujiulize maswali magumu: Je nini kifanyike kuhakikisha watoto wanajifunza? Je, tutaweza kubadilisha matazamo wetu wa elimu na kulenga matokeo kujifunza?

Walimu ni sehemu nzuri ya kuanzia kwa kuwa rasilimaliwatu ni muhimu zaidi. Walimu hupenda mfumo huu wa Malipo baada ya Matokeo kwa kuwa unatoa fursa kwao ya kupata kipato cha ziada. Jambo hili litawapa watunga sera wasaa na uhalali wa kuwadai walimu kuwajibika zaidi kwa kujali zaidi maendeleo ya wanafunzi.

Walimu wenyewe wanaupenda utaratibu wa Malipo baada ya Matokeo; asilimia 95 walipendelea programu hii (na asilimia 75 walipendelea zaidi). Walipoulizwa iwapo wangependa wapewe ongezeko la asilimia 15 la mishahara, ni asilimia 35 pekee ndio waliochagua njia iliyozoeleka ya “kiwango sawa kwa wote”. Lakini asilimia 65 walichagua nyongeza ya malipo inayoendana na matokeo ya kujifunza.

Mwisho, Tanzania imekwishaanza kutekeleza mfumo wa utoaji wa motisha uitwao Ruzuku kwa Maendeleo ya Shule (SIG) tangu mwaka 2014. Tunaamini kuwa huo ni mwanzo mzuri, hata hivyo tunashauri mfumo huo uongezwe makali ili wanafunzi na walimu wengi zaidi wanufaike. Twaweza ipo tayari kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kutekeleza mfumo mzuri wa utoaji motisha, kutokana na uzoefu wake wa muda mrefu katika kutekeleza mfumo wa Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo.

Je, motisha inatosha kuinua kujifunza? Hapana, hii ni sehemu tu ya utata uliopo. Hata hivyo baadhi ya njia za kuinua kujifunza zinaushawishi mkubwa kwa walimu kuzitumia hasa pale wanapoona kuwa njia hiyo inawawezesha wanafunzi wao kujifunza zaidi. Viongozi wa shule na walimu wataanza kutafuta ufumbuzi watakapoona ishara kuwa Malipo ya Walimu baada ya Matokeo ulioinua kuwango cha kujifunza una thamani kubwa.

Pendekezo letu ni kutekeleza mpango wa Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo katika eneo dogo kwanza, tujaribishe na kujifunza; kisha tuchague muundo wa utekelezaji unaofaa zaidi na kuamua kuhusu utekelezaji nchi nzima.